

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

WEWE NI NANI?

(*Habari ifuatayo ni hadithi ya mambo ambayo yamenakiliwa katika Matendo 19:10-20 SUV*).

Paulo mtume wa Yesu Kristo alihubiri katika mji wa Efeso kwa miaka miwili. Katika muda huo alishiriki na watu wa Efeso ujumbe wa ajabu wa wokovu na kuwaambia kuhusu Roho Mtakatifu na pia kuhusu Ufalme wa Mungu. Basi habari njema za injili zikasambaa kote katika Asia Ndogo kwa watu wote, Wayahudi na Wayunani. Ujumbe huo ukaambatana na miujiza ya uponyaji na kukombolewa kwa watu kutoka kwa mapepo chafu jambo ambalo lilidhihirisha ukweli wa ujumbe huo. Basi nguvu za Mungu zikawa juu ya Paulo kwa njia ya ajabu. Yeye basi angeombea vitambaa na kuvipaka mafuta halafu vitambaa hivyo vingepelekewa waliokuwa wagonjwa na waliopagawa na ibilisi nao wagonjwa wakapata kuponywa magonjwa yao na wale wenye pepo chafu wakawekwa huru.

Lakini kulikuwa na Wayahudi kadhaa ambao kazi yao ilikuwa ni kupunga pepo na ambao walienda huku na huku kwa lengo la kutoa pepo wachafu na kuponya magonjwa ya watu kwa kuita mizimu na kwa nyimbo za kumpandisha shetani. Watu hawa waliposikia jinsi Paulo alitoa pepo chafu kwa jina la Yesu wao wakalongezea jina hilo kwa mkusanyo wa misemo na mazoea yao. Basi wakawaambia watu waliopagawa "Nawaapisha kwa Yesu, yule ambaye anahubiriwa na Paulo." Naye Skewa, ambaye alikuwa kuhani mwenye mamlaka kati ya Wayahudi alikuwa na wana saba ambao walikuwa na tamaa za kupata hizo nguvu. Basi waliposikia habari kumhusu Paulo na nguvu ambazo zilikuwa katika jina la Yesu wao walikusanyika na kumzunguka mtu ambaye alikuwa na pepo mchafu. Na huku wakiwa na madahiro na kutaka kujionyesha

walimwekelea mtu huyo mikono na kusema, "Katika jina la Yesu twakwamuru—toka!"

Naye pepo mchafu akazungumza kutoka ndani ya mtu huyo: "Yesu namjua na Paulo namfahamu, lakini ninyi ni nani?" Kwa maneno mengine, "Mimi najua mamlaka ya kiungu ya Yesu akiwa Mwana wa Mungu na pia najua nguvu za Paulo mtumishi wake Yesu, lakini nyinyi hamna uhusiano na Mungu na hamna mamlaka yoyote juu yangu. Nyinyi wenyewe mwadhanu ni akina nani?" Kumaliza kusema hayo pepo mchafu akamwondoka mtu huyo ambaye alikuwa amepagawa na kuwarukia watu hao wa kupunga pepo. Nazo nguvu za Shetani zikawazidi na kuwapagaa na huku wakipaza sauti na kujigongagonga wakaanguka chini na kutoa pofu midomoni mwao halafu wakaruaruarua nguo zao kabla ya kutoroka kutoka nyumba humo huku wakiwa uchi na wakijaa majeraha.

Wakati Wayahudi na Wayunani wa Efeso waliposikia habari hizo woga mwingi ukawaingia na jina la Yesu likapata kutukuzwa. Basi watu wengi wakakiri uovu uliokuwa maishani mwao na wakaokolewa kutokana na nguvu za dhambi. Ndipo wakaleta vitabu vyao vya uganga, vya nyimbo za kuita mizimu na kupandisha shetani, na kuvichoma kwa moto mkubwa sasa wakijua kwamba mambo hayo hayakulingana na matakwa yake Mungu. Na hapo Neno la Mungu likasambaa kwa nguvu wakati watu hawa walikataa kazi za ibilisi.

Mtu akisoma Maandiko kuhusu matukio haya ya ajabu anapata msisimko na himizo kubwa, lakini kusoma mambo hayo kunastahili pia kumletea mtu hali ya kumwogopa Mungu na kumheshimu. Kuna nguvu ndani yake Yesu lakini nguvu hizo zinapatikana na wale

(Endelea katika Ukurasa 2)



"Naye pepo mchafu akazungumza kutoka ndani ya mtu huyo:
'Yesu namjua na Paulo namfahamu,
lakini ninyi ni nani?'"

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)

tu amba wanamfahamu
Mungu vizuri na wenyewe usafi
wa moyo. Shetani mwenyewe
anajua Yesu ni nani na anajua
atumishi wa kweli wa Bwana
ni nani. Yeye anawajua wale
ambao hawajaokoka na pia
anajua dhambi ya siri na
uovu amba umo ndani ya
moyo wa mwanadamu. Yeye
anajua manafiki na wahubiri
ambao maisha yao ni kama
wana wale saba wa Skewa.
Basi pepo mchafu aliuliza

swali ambalo linahitaji kuchunguzwa na kila mtu kwa makini. Wewe
ni nani? Kitambulisho chako ni kipi? Ukweli wa tabia zako ni upi?

Watu wengi hujitambulisha kwa misingi ya jina lao, kabila lao, tabaka
zao, dini zao, kusanyiko lao la kanisa, au vyeo vyao. Lakini mambo
hayo yote sio muhimu yakilinganishwa na kitambulisho cha kiroho.
Kitambulisho hicho cha kiroho hakilingani na sifa za kiroho za mtu au
cheo chake katika uongozi wa kanisa. Kitambulisho hicho kinalingana
na hali halisi ya moyo wa mtu na matendo ya maisha yake.

Je, wewe kweli ni mtoto wa Mungu? Je, unaishi kulingana na
matakwa ya utakatifu na una shauku kila siku ya kumpendeza
Bwana? Je, wewe unajiita Mkristo na pengine una ushirika na watu
wa Mungu lakini una dhambi maishani mwako? Je, wewe huonekana
mtakatifu Jumapili lakini siku zingine za wiki unaishi na kuvala nguo
za kidunia? Je, una furaha ya Bwana maishani mwako? Je, wewe
ni mkweli ama kuna nyakati zingine unakuwa mdanganyifu?

Je, wewe waonekana kuwa mume au mke unayempenda mumewe au
mkewe lakini ambaye anamfanyia madhara mpenzi wake wa ndoa
hapo hapo nyumbani? Je, wewe unaepukana na maovu mchana lakini
u mtu ambaye unafuata tamaa za dhambi na mwili giza likiingia?
Kitambulisho chako cha kweli sio vile ambavyo ulikuwa hapo mbeleni
au vile ambavyo ungalitaka kuwa baadaye. Wewe ni nani kwa sasa?

Siku moja kila mtu atasimama mbele zake Mungu na kuhukumiwa
kulingana na kitambulisho chake cha kweli cha kiroho. Basi
hatuna budi kila mmoja wetu kuchunguza moyo wake na kujiuliza
swali: "Mimi kwa kweli ni nani kwa mambo ya kiroho?" ■


*Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo,
asiwe msikiaji msahafulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri
katika kutenda kwake.*

—Yakobo 4:13

Gazeti la Ukweli wa Injili ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya
Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike
kweli za Biblia. Tudembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili
uve ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze
kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la Ukweli wa Injili linachapishwa katika nchi nyingi ili
lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kuitia kwa matoleo yanayotolewa kwa
hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi
yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org



"Je, wewe unajiita Mkristo ... lakini
unayo dhambi maishani mwako?"

Tahariri



Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo. —Wafeeso 4:13

Wakati mtu ameokolewa na damu ya Yesu na kutakaswa na Roho Mtakatifu yeye hujipata kwamba ameandaliwa kumtumikia Bwana kwa utakatifu.

Kwa kweli bado kutakuwa na mambo ambayo Bwana atakuwa anakamilisha maishani mwake na sehemu ambazo mtoto wa Mungu atahitaji kukua. Lakini mtoto wa Mungu hana haja ya kuogopa kukiri udhaifu wake au sehemu katika maisha yake ambayo hatimizi malengo ya Kikristo maishani mwake. Hii ni kwa sababu ni wakati ambapo tumekiri upungufu wetu ndio tunapata ushindi mkuu zaidi na nguvu za kuishi kama Wakristo. Basi wewe usife moyo wakati Bwana amekuonyesha haja yako ya kiroho. Jambo hilo hutokana na rehema na upendo wake Mungu ili kutusaidia kuijandaa kwa ajili ya hukumu yake.

Katika robo hii ya mwaka somo letu si la kithiolojia kwa maana ni somo la kuwahimiza Wakristo. Mzigo nilio nao wakati huu ni kushiriki baadhi ya maandiko yanayohusiana na haja ya mtu kujichunguza kibinagsi. Ni vigumu sana kwetu mtu kujiona vizuri kwa sababu watu wengi mara nyingi hujitazama kwa mwangaza wa kujipendeza wao wenyewe. Lakini hatutoweza kukua katika Kristo kama hatuko tayari kuchunguza maisha yetu na kuwa watu wa kweli kuhusiana na mahitaji tulio nayo. Mungu kamwe hatawahi kutuuliza kubadilisha kitu maishani mwetu pasipo kutupatia neema na uwezo wa kufanya mabadiliko hayo.

Ulimwengu wetu umejaa watu amba wanakiri jina lake Kristo lakini amba wangali wanaishi dhambini. Je, ni jambo gani lingefanyika kama kila mmoja wetu angepima maisha yake kwa ukweli kulingana na Neno la Mungu pasipo kutoa visingizio au kuwalaumu watu wale wengine? Ni kweli kwamba wenye dhambi wanahitaji kutambua dhambi yao, lakini katika kipindi hiki mimi nina mzigo mkubwa kwa ajili ya watu wanaojiita Wakristo lakini wanaishi maisha hafifu sana yakilinganishwa na Neno la Mungu. Hakuna mmoja wetu ambaye yuko huru kutokana na maagizo ya Neno la Mungu. Watu wengi wanajifanya kana kwamba wanaweza kudumisha miongozo na viwango vyao wenyewe na kumwingiza Mungu humo ndani katika viwango vyao. Lakini Mungu habadiliki, sisi ndio amba tunahitaji kubadilisha maisha yetu ili yalingane na mapenzi yake. Hapo ndipo tunapata amani ya kweli na utoshelevu katika kumtumikia Bwana. Ni jambo la kushusha moyo sana mtu kudai kuwa ni mtoto wa Mungu lakini afiche maovu huku akitumaini kwamba hatapatikana na yejote. Pia ni jambo la huzuni kwamba washiriki wa kusanyiko la Mungu wanaendelea kukosa aibu ya kuishi maisha ambayo ni ya kidunia.

Hata ingawa ni muhimu sisi kuchunguza mafundisho yetu ya kidini na yale tunayoamini, ni muhimu zaidi kuchunguza mielekeo yetu na mambo ambayo tunayapenda. Watu wanaweza kuwa na mafundisho bora lakini pia wawe na mielekeo au mambo maishani mwao ambayo hayampendezi Mungu. Basi hebu tufungue mioyo yetu kwa Roho wake Mungu. Hebu tuwe makini wakati tunasoma Biblia na kusikia jumbe kutoka kwa watumishi wa Mungu waliopakwa mafuta. Tunapojichunguza maisha yetu na kumfuata Kristo ndipo tutakuwa na ujuzi zaidi wa utimilifu wa Kristo maishani mwetu.

Mhariri, Michael Smith.

Januari 2018



Tutembelee

www.thegospeltruth.org

ili kujandikisha na

kupata jarida

za mbele.

Mwongozo wa Kujifunza Biblia

Somo: Kujichunguza Kibinafsi



Somo la Biblia: *Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe.* —2 Wakorintho 13:5a

Maana: Mtu kujichunguza mwenyewe ni somo na uchunguzi wa tabia zako mwenyewe, sifa zako, jinsi unavyoendesha maisha yako, na malengo ya moyo wako; kujichunguza kindani.

Muhstasari: Ni jambo muhimu mtu kuchunguza maisha yake ya kiroho ili asifike mahali pa kujihesabia haki na basi kuwa mnafiki, kujikinga dhidi ya kuwa watu waliodanganyika, na mwishowe kukosa kufika mbinguni.

I. Jichunguze Mwenyewe

- A. 2 Wakorintho 13:5 Maagizo ya kujichunguza kibinafsi.
- B. 1 Wakorintho 11:27-31 Jihukumu mwenyewe.
- C. Zaburi 77:6 Kutafuta kwa makini.

II. Umuhimu wa Kujichunguza Mwenyewe

- A. 1 Wakorintho 10:12 Ili usije ukaanguka.
- B. Warumi 4:12-13 Kuwajibika kwa Mungu
- C. Mithali 21:2 Machoni petu wenyewe
- D. Wagalatia 6:7-8 Mavuno ya milele.
- E. 1 Wakorintho 6:9-11 Uovu unalaaniwa.

III. Kujidanganya Mwenyewe

- A. Mithali 30:12 Kuwa safi machoni pao wenyewe.
- B. Yakobo 1:22-25 Msikilizaji anayesahau kwa haraka.
- C. Wagalatia 6:3-4 Kiburi ni cha kujidanganya wewe mwenyewe.
- D. Mathayo 7:1-5 Ondoa kibanzi chako.

IV. Kujihesabia haki

- A. Mithali 20:6-7 Kujihesabu kwamba wewe ni mtu mzuri.
- B. Luka 16:15 Kujihesabia haki.
- C. 2 Wakorintho 10:17-18 Kujisifu wewe mwenyewe.
- D. Mathayo 3:7-9 Usitegemee uzao wako.

V. Kujihesabia haki

- A. Mathayo 5:20 Hamtaingia mbinguni.
- B. Mathayo 23:2-8 Wanasema lakini hawatendi.
- C. Mathayo 23:23-29 Manafiki. Utakatifu wa kuonekana tu.

VI. Mambo ya Siri

- A. Yohana 3:19-21 Nuru humurika.
- B. Mhubiri 12:13-14 Mungu atahukumu.
- C. Mithali 28:13 Kuficha dhambi.

VII. Jihukumu Mwenyewe Kulingana na Tunda la Maisha Yako

- A. Mithali 20:11 Mtoto hujulikana kwa matendo yake.
- B. Mathayo 7:13-23 Mti mwema huzaa matendo mema.
- C. Yohana 10:27 Kondoo hufuata Mchungaji.
- D. Tito 2:7-8 Kielelezoo cha matendo mema.
- E. Mathayo 25:33-46 Matendo mema.

VIII. Jichunguze Kabisa Kabisa

- A. Yohana 21:15 Ni nini unapenda sana?
- B. 1 Wakorintho 6:20 Mtukuze Mungu katika mwili na roho.
- C. 2 Mambo ya Nyakati 25:1-2 Shauku za moyo.

IX. Mruhusu Mungu Akuchunguze

- A. Zaburi 26:2 Bwana nijaribu na unipime.
- B. Zaburi 139:23-24 Ee Mungu, unichunguze.

X. Yakiri Mahitaji Yako

- A. 2 Samueli 12:7 Wewe ndiwe mtu huyo.
- B. 2 Samueli 12:13 Nimefanya dhambi.

XI. Dumisha Uwazi Mbele Zake Mungu

- A. 2 Wakorintho 7:10-11 Jichunguze.
- B. Matendo 24:16 Dhamira safi.
- C. 2 Wakorintho 7:7 Kutimiza utakatifu.
- D. 2 Petro 3:18 Kukua katika neema.

Tamati

Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa. —2 Petro 3:11

Faida za

KUJICHUNGUZA KIBINAFSI

kwa Mamba ya Kiroha

Huku ikijulikana kwamba siku ya hukumu yaja Maandiko yametilia umuhimu swala la mtu kujichunguza tabia zake mwenyewe, jinsi anavyoendesha maisha yake, na misukumo inayofanya kazi maishani mwake. Ni bora zaidi mtu kujipima akiwa maishani haya kwa misingi ya Neno la Mungu huku kukiwa kungali na nafasi ya kufanya hivyo, badala ya yeye kusubiri hukumu yake Mungu wakati ambapo mtu atakuwa amechelewa kabisa.



“Pasipo mtu kujichunguza kwa kuongozwa na mwelekeo wa kumwogopa Mungu yeye atajipata kwamba amejihadaa mwenyewe.”

“Basi ni hivyo, kila mtu mionganini mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu”(Warumi 14:12). Siku moja tutasimama mbele yake Mungu hapo siku ya hukumu na kuwajibika kwa ajili ya maisha tulioishi humu duniani. Wakati huo hatutahukumiwa kulingana na yale tuliofanyiwa na wengine, au kulingana na manthari iliyotuzunguka maishani. Kwa kweli tutahukumiwa kulingana na hali ya mioyo yetu na kulingana na maamuza yetu ya kila siku na pia kulingana na tabia zetu.

Jichunguze Mwenyewe

Hata ingawa ni rahisi zaidi mtu kuona dhambi na makosa ya watu wale wengine mtume Paulo alihimiza kanisa la Korintho “Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe” (2 Wakorintho 13:5). Usitazame maisha ya wengine na badala yake chunguza maisha na imani yake. Waza kuhusu moyo na roho yako kwa makini (Zaburi 77:6) na ujihakikishie kwamba una ujuzi wa kibinafsi na Mungu. Ukweli kwamba mtu amemtumikia Bwana miaka mingi si kumaanisha kwamba kwa sasa anaishi maisha yanayompendeza Mungu. “Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke” (1 Wakorintho 10:5).

“Kila njia ya mtu ni sawa machoni pake mwenyewe; bali Bwana huipima mioyo” (Mithali 21:2). Ni rahisi zaidi mtu kuchukulia kwamba yu sawa na kwamba wengine wamepotoka kuliko yeye kuchunguza maisha yake kwa ukweli. Mungu hushughulishwa sana na swala la kuchunguza (sio tu tabia za mtu) bali hasa shauku za moyo wake. Basi ni jambo la busara sisi kuchunguza maisha yetu ya kibinafsi ili tuweze kujua vile Mungu angalitaka tuwe

badala ya kufuata kile ambacho mwili wetu umekubali na kuruhusu. Kwa kweli kile ambacho tutapanda maishani haya ndicho tutavuna milele. Usidanganyike, hatuwezi kumpumbaza Mungu, kwa maana Yeye ajua mambo yote (Wagalatia 6:7-8). Maandiko yanafundisha kwa njia ya wazi kabisa katika 1 Wakorintho 6:9-11 kwamba waovu hawataingia Mbinguni. Waasherati, wazinzi, mashoga, wevi, walevi, waongo n.k. watateseka milele ikiwa hawatamrudia Mungu na kuishi maisha matakatifu. Ulimwengu umejaa watu wanaojidai kuwa ni Wakristo lakini ambao wanatenda dhambi hizo. Mwisho wao ni wa hakika kama hawatatabu. Kuna kizazi ambacho kinajihesabia haki machoni pao wenyewe lakini kingali bado hakijaoshwa kutokana na uchafu wa maisha yao (Mithali 30:12).

Hatari ya Kujidanganya Mwenyewe

Pasipo mtu kujichunguza kwa kuongozwa na mwelekeo wa kumwogopa Mungu yeye atajipata kwamba amejihadaa mwenyewe. Haitoshi kusikia Neno; ni lazima tuwe watendaji wa Neno au tutajihadaa wenyewe (Yakobo 1:22-25). Mtu kujua ukweli kiakili na kuwa na ushirika na watu wa Mungu haitoshi kumuandaa kwa ajili ya hukumu yake Mungu. Baadhi ya watu ambao wanaona wale wengine wana makosa ni wale ambao wana kibanzi machoni mwao; “Itoe kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe; ndipo utakapoona vema kukitoa kile kibanzi katika jicho la ndugu yako” (Mathayo 7:1-5).

Epukana na Kujihesabia Haki

Ni jambo la baraka mtu kwenenda kwa uadilifu na kuishi kwa uaminifu. Huu ni mwenendo ambao ni tofauti na watu ambao hujitangazia wema wao wa kibinafsi (Mithali 20:6-7). Kujitangazia kuwa wewe ni mtakatifu hakumwokoi mtu na pia kujidai kwa mambo ya kiroho hakumletei mtu nguvu kutoka kwa Mungu. Yesu akasema: “Ninyi ndinyi mnaojidai haki mbele ya wanadamu, lakini Mungu awajua mioyo yenu” (Luka 16:15). Lakini mtu kujifanya uchunguzi wa kibinafsi sio kujihesabia haki, “Maana mtu mwenye kukubaliwa si yeye ajisifuye, bali yeye asifiwaye na Bwana” (2 Wakorintho 10:18). Kuna watu wengi ambao hutoa visingizio vyamambayo yako maishani mwao, mambo ambayo hayakubaliwi na Mungu. Watu wengine huweka tumaini lao kwa jina la familia, kabilia lao, kanisa lao, historia yao, au cheo chao uongozini. Lakini Yohana Mbatizaji

(Endelea katika Ukurasa 6)



**"Jinsi mtu alivyo
na ukweli na
uwazi mbele zake
Mungu ndivyo
atakavoendelea
kukua kiroho
bila kukoma."**

lakini wakawa watu wa kimwili ambao walijaa maovu. Ndipo Yesu akawaita manafiki. Hata ingawa mtu kuva mavazi ya kiwango cha wastani ni jambo muhimu na ambalo linastahili kufundishwa, lakini kilicho muhimu zaidi ni uchunguzaji wa mtu kwa ndani. Kuna watu ambao kwa nje wanaonekana watatifu lakini roho zao zimejaa uchoyo, kiburi na chuki. Basi jichunguze.

Hakuna Kilichofichika

Tunahitaji kujipima kwa kutumia mwangaza wa ukweli badala ya kuendelea kukaa katika blanketi ya giza, blanketi ya kujihesabia haki, na ya utakatifu wa kibinafsi. Mungu atahukumu kila neno la siri (Mhubiri 12:13-14). Basi fanya uchunguzi kuhusu maisha yako na usitoe visingizio kwa chochote ambacho hakilingani na uungu. Watu wakificha dhambi hawatanawiri. Lakini wakikiri dhambi yao na kuachana nayo ndipo Mungu atawarehemu (Mithali 28:13).

Kujulikana kwa Tunda Lako

Mithali 20:11 inasema: "Hata mtoto hujijulisha kwa matendo yake; kwamba kazi yake ni safi, kwamba ni adili." Kama ambavyo mtoto anajulikana ndivyo ambavyo tunahitaji kujitambulisha kwa ukweli wa matendo yetu. Je, wewe unazaa tunda la aina gani? Yesu alisema kwamba mti mzuri huzaa matunda mazuri (Mathayo 7:16-23) na kwamba tutawajua wengine kwa matunda yao—vivyo hivyo ndivyo tunastahili kujijua. Ni jambo la baraka

(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)

aliwaambia Mafarisayo: "Wala msiwaze miyoni mwenu kwamba, Tunaye baba, ndiye Ibrahim" (Mathayo 3:9). Wao walijiona kuwa watakatifu kwa sababu walikuwa wazaliwa wa watu watakatifu (wa kale). Tunaweza kuwa na wazazi na mababu ambao walimfanya Mungu kazi sana. Tunaweza kuwa washirika wa ibada za "Kanisa la Mungu," lakini jambo hilo halituokoi wala kutufanya kuwa wenye haki ikiwa tunafanya uovu maishani mwetu.

Jichunguze Kindani

Dini na ibada za kuonekana kwa nje hazituokoi. "Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni" (Mathayo 5:20). Katika Mathayo 23:23-29 Yesu alisema mengi kuhusu utakatifu wa kibinafsi wa viongozi wa kidini wa wakati wake. Wao walisema maneno yaliyofaa lakini hawakufuata sheria yake Mungu.

Wakavalia mavazi ya utakatifu

kubwa mtu kuchunguza maisha yake mwenyewe na kuona kwamba analo tunda nzuri. Lakini pia Yesu alitoa onyo dhidi ya mbwa mwitu wanaovaa vazi la kondoo. Kuna wahudumu wa Injili ambao wametuzunguka na ambao wanahubiri na kusema kwamba wana nguvu kutoka kwa Mungu lakini kwa kweli wao ni mbwa mwitu wa kiroho. Lakini kondoo wa kweli wana uhakika na usalama wakati wanachunguza maisha yao, kwa maana kondoo wanajua sauti ya mchungaji wao na wanamfuata (Yohana 10:27).

Chunguza Mwili na Roho Yako

Mtu kamili anahitaji kuchunguzwa, ndani na nje. Yesu alimuuliza Petro: "Jel Simoni wa Yohana, wewe wanipenda kuliko hawa?" (Yohana 21:15). Je, wewe wampenda Mungu kuliko kitu kingine chote ulimwenguni? Je, wewe watafuta mambo ya kilimwengu au Kristo ndiye aliye muhimu zaidi maishani mwako. Katika 1 Wakorintho 6:20 tumeagizwa kwamba tumtukuze Mungu katika miili na roho zetu. Wakati mtu anatazama kioo ye ye huona mfano wake kwenye kioo hicho. Basi Wakristo wanahitaji kutazama kioo cha kiroho na kuchunguza uhalisi wao kwa mambo ya kiroho, huku wakipima maisha yao kulingana na kiwango cha Neno lake Mungu.

Mruhusu Mungu Akuchunguze

Mfalme Daudi alitoa mfano kwetu katika maombi yake ya kila mara: "Ee Mungu, unichunguze, uujuwe moyo wangu, unijaribu, uyajue mawazo yangu" (Zaburi 139:23-24). Wakati nabii Nathani alimkaripia Daudi kwa ajili ya dhambi yake Daudi alikubali dhambi yake na kutafuta msamaha. Basi hebu tufungue miyo yetu na kumruhusu Mungu kutuchunguza ili atuonyeshe chochote ambacho hakilingani na Kristo. Inaweza kuwa ni udhaifu (ambao pengine hata sio dhambi) lakini ambao unatuzaia kukua kiroho. Basi jichunguze na kupata ushindi kupitia kwa kukiri dhambi zako na kubadilisha maisha yako.

Moyo Ulio Tayari

"Na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu" (2 Wakorintho 7:1). Basi jitakase mbele zake Mungu na kila siku ufanye juu chini kama mtume Paulo ili uwe "na dhamiri isiyo na hatia mbele za Mungu na mbele ya watu siku zote" (2 Wakorintho 7:1). Jinsi mtu alivyo na ukweli na uwazi mbele zake Mungu ndivyo atakavoendelea kukua kiroho bila kikomo.

Furaha ya Mtu Anayejitolea Kikamilifu

Kuna amani ya ajabu ambayo mtu upata anapotambua kwamba dhambi zake zimesamehewa, kwamba moyo wake ni safi, na kwamba shauku ya moyo wake ni kumpendeza Mungu. Ni ushuhuda wa ajabu mtu kuweza kusema (kama Yesu) kumhusu Shetani: "Yeye hana kitu kwangu" (Yohana 14:30).

Kwa sababu mwisho wa mambo yote uko karibu tunahitaji kuwa watu wa aina gani? Basi tusiogope kujichunguza kibinafsi kwa maana kuna Mungu ambaye yuko tayari kutuhudumia kulingana na mahitaji ya maisha yetu. ■

Swali

na

Jibu

Je, ni nini maana ya “bahari ya kioo” ambayo inazungumziwa katika Ufunuo 4:6?

Maandiko yanasema: “Na mbele ya kile kiti cha enzi kulikuwa na mfano wa bahari ya kioo, kama bilauri; na katikati ya kile kiti cha enzi, na pande zote za kile kiti, walikuwako wenye uhai wanne, wamejaa macho mbele na nyuma.”

Ufunuo 15:2 nayo inasema kuhusu bahari ya kioo na kuchora mchoro ambao unafanana na ule wa Ufunuo 4:6. Kile ambacho kinatiliwa mkazo katika maandiko hayo ni urembo na utukufu wake Mungu katika kiti chake cha enzi ambacho kina utukufu. Watakatifu wote wa nyakati zote wamekusanyika na kukizunguka kiti cha enzi huku wakimwabudu na kumsifu Bwana Mungu wa Majeshi.

Maandiko hayo yanastahili kuchunguzwa ili watu waweze kuyaelewa, lakini kwa sasa mimi nitashughulikia tu swali ambalo limeimbuka.

Bahari ya kioo ilikuwa kama bilauri na ilikuwa imetandazwa mbele ya kiti cha enzi. Bahari hii ilikuwa yenyewe uwazi kama kioo maanake mtu angeweza kuona “upande ule mwengine” bila kizuiji kama ambavyo mtu anaweza kuona kupitia kwa kioo. Ni kwenye bahari hii ndipo waliokombolewa walismama na kumwabudu Mungu. Lakini jambo hili halistahili kuelewaka kama lililotendeka kwa uhalisi bali ni kwa njia ya mfano. Ni jambo bora kwamba kiti cha enzi kimezungukwa na bahari ya kioo kilicho wazi, safi, bila ila, na kujaa utakatifu. Bahari na kioo hicho kinawakilisha ukweli, utakatifu, na uwazi. Kanisa lililo la kweli limesimama bila ila au lawama na linaishi kwa usafi na upendo.

Hata katika siku zetu, wakati ambapo watakatifu wangali duniani, wao wanahitaji kusimama juu ya bahari ya kioo ambako hakuna chochote kilichofika au kufunkwa. Sisi tuko kama tunavyosema tulivyo, na hatuna haja ya kuficha chochote, kutoa vijisababu, au kutoa visingizio vya kufanya uovu. Ikiwa Wakristo, makusanyiko ya Wakristo, au wahudumu wa injili hawaishi kwa uwazi, basi kuna shida na mambo yanakwenda mrاما. Ndiposa tunahitaji kuinua sauti zetu na kumsifu Mungu kwa njia ya utakatifu na kusimama wima kwa uwazi na usafi katika utakatifu huo wa Mungu. ■



MWONGOZO WA MTU KUJICHUNGUZA KIBINAFI

Je, Mimi . . .



Nampenda Mungu kwa moyo wangu wote?

KILA WAKATI	WAKATI MWINGINE	LA, HASHA
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>

Namtii Mungu kwa kila sehemu ya maisha yangu?

Nasema kwa maneno ya neema na upendo?

Navaa mavazi ya kiwango cha wastani na urahisi?

Ni mwenye unyenyekevu kuhusiana na jinsi ninavyojiona mwenywewe?

Ni mwaminifu kuhudhuria ibada za kanisa?

Ninajaribu kuficha kitu maishani mwangu?

Natazama au kusikiliza mambo ambayo ninaweza aibika machoni pake Kristo?

Niko makini kufanya maombi na kusoma Biblia?

Ni mtu mtakatifu hapo nyumbani kama nilivyo katika ibada za kanisa?

Nadhirisha roho na usafi wa Kristo?



JE, WAJUA?

Jinsi ambavyo biblia inatumia neno "mnafiki" (kama liliyotumiwa na Yesu) ni tofauti na lina maana zaidi kuliko jinsi linavyotumika leo. Katika siku zetu neno hilo lina maana ya mtu kusema jambo moja na kutenda jambo lingine, yaani mtu mwenye nyuso mbili, mtu asiyeminika. Lakini kiini hasa cha neno hilo kwa lugha ya Kiyunani linaashiria "watu wa kuigiza kwenye jukwaa." Mchezaji wa michezo ya kuigiza alifanya juu chini ili aweze

kutambulika, kukubalika, na kupigwa makofi na wanadamu. Lakini wakati hamna mtazamaji, wakati watazamaji wamerudi makwao, mwigizaji huyo hurudia hali yake ya kawaida, ambayo mara nyingi ni tofauti kabisa na wajibu aliokuwa akiigiza kwenye uigizaji wake katika mchezo huo wa kuigiza.



MKARIBISHANE NINYI KWA NINYI

Kwa hiyo mkaribishane ninyi kwa ninyi, kama naye Kristo alivyotukaribisha, ili Mungu atukuzwe. —Warumi 15:7

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

Kristo amewanyoshea mkono wa urafiki na makaribisho watu wa mataifa, lugha na tabaka mbali mbali. Yeye amewakubali watu wa tabia tofauti na uzao tofauti. Yeye alitupokea katika hali yetu ambayo ilikuwa imezoroka na katika umaskini wetu. Kwa upendo wake Yesu alitufikia katika upotevu wetu na kutuinua kwa neema yake. Hata ingawa wokovu wa Mkristo huleta mabadiliko makubwa maishani mwake yeye hubaki na maumbile yale yale ambayo yanakanganya hata baada ya kuokoka. Kusema kweli sisi huwa tunabaki na maoni yetu ya kibinadamu, na hata udhaifu wetu unaendelea kuwa nasi. Hata hivyo Kristo hutupokea na kutukubali kwa upendo wake mkuu. Kutokana na hayo sisi tunafanya watu wasio wa nje, hatuwi wageni tena, bali tunakuwa washirika wa Ufalme wa Mungu.

Jinsi ambavyo Kristo alitupokea ndivyo tunahitaji kukaribishana. Tunahitaji kufungua mioyo yetu kwa Wakristo wenzetu na kuwashughulikia kwa upendo na hesima kama ndugu na dada zetu katika Bwana. Kwa kweli Kristo hakutupokea kwa sababu ya ukamilifu wetu bali kwa sababu ya kutokamilika kwetu. Je, tunawezaje kutumia kiwango hafifu zaidi katika mahusiano na wenzetu? Basi tunahitaji kuwa na uhusiano wa upendo na wa kiungu na wenzetu na kuwakubali badala ya kujitenga nao au kujenga ukuta dhidi yao kwa sababu ya tofauti ndogo ndogo za maumbile na maoni. Je, kama Kristo angalitupokea vile tunapokea wenzetu kwa mambo ya kiroho kwa kweli tungalikuwa na ushirika naye?

Basi hatustahili kuwatenga au kuachana na Wakristo wale wengine kwa sababu tumehisi kwamba wao ni dhaifu kwa mambo ya imani au katika uelewaji wao wa Ukristro. Mtume Paulo alitoa mawaidha na kusema: "Yeye aliye dhaifu wa imani, mkaribisheni, walakini msimhukumu mawazo yake" (Warumi 14:1). Hapa mtume Paulo alikuwa akizungumzia Wayahudi amba walikuwa wameokoka na amba walikuwa wakiendelea kushikilia sehemu fulani za Sheria ya Musa. Mwongozo alioutoa ni kwamba Wakristo walistahili kuwapokea na kuwakubali Wayahudi hao katika ushirika wa kidini. Halafu pia akawaagiza Wakristo kuwapokea watu kama hao bila kuzua mgogoro na mabishano ya kidini. Akawaambia kwamba wasiabague au kuwaleta kwa ushirika wakiwa na kusudi la kuwalaani au kwa ajili ya kufanya mjadala mkali nao. Basi akawaomba kuwapokea kwa mikono miwili na kwa upendo.

Ni jambo la kushangaza kwamba kati ya watoto wa Mungu washirika wawili wanaweza kuona kwamba yule mwingine ndiye mwenye udhaifu katika imani. Wakati mwingi Wakristo (ambao ni mabaki madogo ya Ukristro) huangaliana kwa macho ya tuhuma na maswali. Lakini Maandiko yanatufundisha kwamba tuwe tayari kupokeana badala ya kutupana nje. Basi, "Mkaribishane ninyi kwa ninyi. ■

